SHIRIKA LA RELI TANZANIA


# RELI na MATUKIO

Gazeti
Kila Mwezi



Agosti 03, 2020

Gazeti la Reli | Toleo Namba 9 | Habari | Makala | Matukio | Elimu | Picha



# TRC YAOMBOLEZA KIFO CHA HAYATI BENJAMIN WILLIAM MKAPA

Na Mwandishi wetu TRC

Shirika la Reli Tanzania limeungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli na watanzania wote kwa ujumla katika maombolezo ya siku saba kufuatia kifo cha Hayati Benjamin William Mkapa, Rais wa tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kilichotokea usiku wa kuamkia tarehe 24 Julai 2020. Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa TRC kwa kutambua mchango wake kwa Shirika na Taifa kwa ujumla katika harakati zake za kuikomboa Tanzania kiuchumi, kijamii na kisiasa wanashiriki kikamilifu katika kumuombea na kumuenzi Rais Mstaafu Benjamin Mkapa kwa mazuri aliyoifanyia nchi yake.

>> Inaendelea Uk. 2

Na Mwandishi wetu TRC Inatoka Uk 1 

# TRC YAOMBOLEZA KIFO CHA HAYATI BENJAMIN WILLIAM MKAPA



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa (kushoto) akipita mbele ya jeneza la Rais Mstaafu wa awamu ya tatu ya Serikali ya Jamhuri Muungano wa Tanzania Hayati Benjamin William Mkapa kwa ajili ya kuaga na kutoa Heshima za mwisho katika uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salam hivi karibuni Julai 2020

Mchango wa Hayati Benjamin William Mkapa ni mkubwa katika taifa kwani yeye ni miongoni mwa viongozi waliothubutu kurejesha Jumuiya ya Afrika Mashariki - EAC kwa maono ya wazee wetu waliyokuwa nayo mara baada ya kupata uhuru, Jumuiya ya Afrika Mashariki imekuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha uchumi wa nchi hizi kupitia sekta ya usafiri wa reli

Mafanikio tuliyo nayo hivi leo ya kusafirisha mizigo baada ya kurejeshwa kwa safari za treni kati ya Dar es Salaam na Kampala ni jitihada za Hayati Benjamin William Mkapa katika kurejesha Jumuiya hii.

Hapo awali Viongozi wa nchi tatu za Afrika Mashariki ambazo ni Kenya, Uganda na Tanzania mara baada ya kupata uhuru waliamua kuunda Jumuiya ya Afrika Mashariki ('East Africa Community') mwaka 1967 kwa lengo la kuunganisha nguvu katika nyanja za usafirishaji na mawasiliano. Ambapo, Shirika la Reli na Bandari Afrika Mashariki lililokuwa wakati wa Ukoloni lilitenganishwa na kuundwa taasisi mbili zinazojitegemea za Shirika la Reli Afrika Mashariki ('East Africa Railways Corporation') na Shirika la Bandari Afrika Mashariki ('East Africa Harbours Corporation'). Shirika la Reli Afrika Mashariki lilianzishwa rasmi tarehe 1 Juni, 1969 ambapo madhumuni yake makuu yalikuwa na usafirishaji wa mizigo na abiria kwa nchi wanachamna na nchi jirani (landlocked).

Ili kupata kiunganishi kizuri cha usafiri wa abiria na mizigo kwa nchi jirani, Shirika la Reli lilitumia usafiri wa majini (meli) kupitia maziwa ya Victoria, Nyasa na Tanganyika. Baadhi ya meli zilizotumika ni MV Victoria, ziwa Tanganyika lilikuwa na meli za MV Liemba, Mwongozo na Sangara, ziwa Nyasa lilikuwa na meli za MV Iringa na MV Songea.

Katika wakati huo Jumuiya ya Afrika Mashariki ilileta ufanisi mzuri wa usafirishaji wa abiria na mizigo kutoka nchi moja hadi nyingine lakini baadae mwaka 1977 Jumuiya hii ilivunjika na kupelekea kila nchi kuanzisha shirika lake, ndipo lilipoanzishwa rasmi Shirika la Reli Tanzania.

Lakini kwa maono hayo Hayati Benjamin William Mkapa alifanya jitihada za kuhakikisha Jumuiya ya Afrika Mashariki inafufuliwa na kuendelea na kazi zilizokuwa zikifanywa wakati wa kuanzishwa kwake, aidha Hayati Benjamin Mkapa alifungua njia ya Reli ya Manyoni – Singida mwaka 1997 ambayo ilisaidia kwa kiasi kikubwa kusafirisha mizigo na abiria.

# TRC YASHIRIKI MAONESHO YA 44 YA KIMATAIFA YA BIASHARA - SABA SABA






Na Mwandishi wetu TRC

Shirika la reli Tanzania – TRC lashiriki maonesho ya kimataifa ya 44 ya biashara yaliyofanyika katika viwanja vya saba saba vilivyopo Kurasini Dar es Salaam kuanzia tarehe 01 - 13 Julai 2020.

Malengo ya maonesho hayo ni kutangaza huduma na bidhaa za kampuni na taasisi binafsi na za serikali, kuwakutanisha watoa huduma na wateja pamoja na kutoa fursa kwa wananchi kupata huduma na bidhaa yalifunguliwa rasmi na Waziri Mkuu wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Kassim katika ukumbi wa Kawawa tarehe 03 Julai 2020.

Shirika lilipata fursa ya kutoa elimu kuhusu miradi mikubwa inayosimamiwa na TRC ambayo ni ujenzi wa reli ya kisasa – SGR kipande cha Dar es salaam – Morogoro ambao umefika zaidi ya 84% na kipande cha Morogoro – Makutupora ambao umefika zaidi ya asilimia 32%, na mradi wa uboreshaji wa reli ya kati – TIRP ambao umefika zaidi ya 80%, pamoja na mradi wa ufunguaji wa njia ya reli kati ya Moshi – Arusha, kutoa huduma ya ukataji tiketi za treni pamoja na kukusanya maoni kutoka kwa wadau
waliofika katika banda la TRC. Halikadhalika wananchi waliotembelea walipata ufahamu kuhusu historia ya reli nchini tangu kuanza kujengwa kwa reli ya zamani wakati wa ukoloni hadi hivi sasa.

Katika maonesho hayo Kaimu Mkurugenzi wa Shirika TRC Bi. Amina Lumuli alitembelea banda la TRC ambapo alifurahishwa na utoaji huduma wa maaafisa wa TRC waliokuwemo katika banda hilo na kuwapongeza kwa kazi nzuri waliyofanya na kuliwezesha Shirika kushinda nafasi ya tatu katika mashindano yaliyofanyika viwanjani hapo.

Pamoja na kutembelewa na wananchi wengi zaidi pia Mchimbaji aliyepata mawe makubwa zaidi ya Tanzanite Bilionea Saniniu Laizer alitembelea na kupata fursa ya kufahamu mambo tofauti kuhusu shirika la reli na kuona mfano wa reli ya kisasa – SGR itakavyokuwa pamoja na maendeleo ya mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR.

Hata hivyo wananchi walifurahishwa na utoaji huduma wa TRC katika banda la shirika ambapo wananchi walihudumiwa na kuweza kutoa maoni yao katika sanduku la maoni na shirika kuahidi kuyafanyia kazi mapendekezo na maoni.

Maonesho hayo yalifungwa rasmi tarehe 13 na Waziri wa viwanda na Biashara wa Zanzibar Mhe. Balozi Amina Salum Ali na kusisitiza wananchi kuendelea na shughuli za uzalishaji wa bidhaa na uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo ili kuendelea kuwa nchi ya uchumi wa kati, aliwasisitiza wanawake kuchangamkia fursa zinazojitokeza.




Na Mwandishi wetu TRC

# TRC YATOA ELIMU YA UKATAJI TIKETI MTANDAONI KWA ABIRIA

Shirika la Reli Tanzania – TRC ni miongoni mwa taasisi kubwa za Serikali ambazo zimefanikiwa kutoa huduma kwa wateja kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) hasa katika ukataji tiketi kwa njia ya mtandao (online booking).

Ripoti ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania - TCRA ya Desemba 2017 imeonesha kuwa idadi ya watumiaji wa mtandao imeongezeka kufikia watu Milioni 23 ambayo ni sawa na 45% ya watanzania wote. Idadi hiyo inaonesha dhahiri kuwa mfumo mpya wa ukataji tiketi kwa njia ya mtandao ni fursa kwa wateja wetu ambao wanatumia mtandao.

Mapema baada ya Shirika kutambulisha mfumo huo, jitihada zilifanyika nje na ndani ya Shirika kuhakikisha mfumo huo unafahamika kwa wateja na wanaweza kuutumia. Julai 16 – 19, 2020 Shirika la Reli nchini kupitia kitengo huduma kwa wateja kiliendesha zoezi la kutoa elimu kwa abiria kuhusu mfumo mpya wa ukataji tiketi kwa njia ya mtandao ndani ya treni ya Deluxe wakati wa safari kutoka Dar es Salaam - Kigoma na kutoka Kigoma – Dar es Salaam.

Shirika linaendelea kutoa elimu hiyo kwa wateja kwa kutumia njia mbalimbali za mawasiliano ikiwemo matangazo ya Redio, Televisheni na Mitandao ya Kijamii lakini pia kupitia machapisho ili kuweza kuwapunguzia changamoto katika upatikanaji wa tiketi wakati wanapotaka kusafiri.

Upatikanaji wa tiketi kwa njia ya mtandao utawasaidia wateja wetu  kuokoa muda waliokuwa wanatumia kufika katika stesheni kwa ajili ya kupata tiketi na hivyo muda huo watautumia katika shughuli nyingine za kiuchumi na kuongeza makusanyo ya mapato kwa kuziba mianya ya upotevu wa fedha.

Aidha wakati wa safari elimu iliendelea kutolewa kwa nadharia na vitendo, huku abiria wakilipongeza Shirika kwa kutambulisha mfumo huo mpya ambao unarahisisha ukataji na upatikanaji wa tiketi hivyo wanategemea itakuwa suluhisho la changamoto nyingi walizokuwa wanakutana nazo awali katika upatikanaji wa tiketi.

Katika kuhakikisha kuwa ukataji wa tiketi kwa njia ya mtandao unawafikia wateja kwa haraka na urahisi, elimu hiyo ilitolewa pia kwa wakuu wa stesheni, makarani na wahudumu wa treni ili kuwapa uwezo wa kuwasaidia abiria wanaofika katika stesheni na abiria pindi wanapokuwa safarini.

# WANAKIJIJI MKADAGE: TUTALINDA MIUNDOMBINU YA RELI

Na Mwandishi wetu TRC

Shirika la Reli Tanzania - TRC limendelea na kampeni ya ushirikishwaji wa jamii katika maendeleo ya mradi wa uboreshaji wa reli ya kati kuanzia Kilosa hadi Isaka, Julai 2020 hivi karibuni.

Maafisa wa maswala ya jamii, wakandarasi kutoka kampuni ya CCECC, pamoja na wafanyakazi wengine kutoka TRC wametembelea maeneo mbalimbali yanayopitiwa na mradi huo ili kufahamisha umma kuwa mradi huo unakaribia kufika ukingoni hivyo kushirikisha wananchi katika kuweka mambo sawa kabla ya ukarabati kukamilika.

Maeneo yaliyofanyika kampeni hiyo ni pamoja na Kilosa kijiji cha Munisagara, Mkadage, Kilosa stesheni, Kidete na Zuzu stesheni, Mnase, Igandu, Kikombo, Godegode vilivyopo mkoani Dodoma.

Aidha wananchi wa kijiji cha Mkadage pamoja na viongozi wa Serikali ya kijiji hicho wameahidi kuilinda miundombinu na mali za reli katika maeneo yao na kusisitiza kua mtu yeyote atakae kiuka taratibu za reli atachukuliwa hatua na kufikishwa sehemu husika.

Mwenyekiti wa kijiji cha Mkadage Bw. Mohammed Kikologa amesema kuwa kwa kushirikiana na uongozi wa kijiji hicho watasimamia wanakijiji pamoja na kutoka elimu juu ya kutunza miundombinu ya reli .

“Sisi ndio walinzi wa kuu wa reli hii ila kukumbushana ni wajibu” alisema Bw. Kikologa.

Afisa wa maswala ya jamii kutoka CCECC Bw. Regan Israel amesisitiza kuwa mwananchi yeyote ahakikishe kutosogea ama kufanya shughuli za kijamii karibu na umbali wa mita zilizopimwa kando mwa reli .

“Mita zilizopimwa ni 30 kutoka katika eneo la njia ya reli“, akaongezea kuwa“ ukiona mtoto, mzee au mtu asiyejiweza mshike mkono na umsaidie kuvuka“ alisema Bw. Regan.

Naye Afisa mazingira kutoka TRC Bw. Evance Byarushengo amewataka wananchi kutojihusisha na maswala ya ukataji miti na shughuli za kilimo kando ya mito ili kuepusha athari zitokanazo na maji kujaa na kuisomba miundombinu ya reli



# ALIYEKUWA MKUU WA MKOA WA DAR ES SALAAM NA WASANII KUTOKA WCB WATEMBELEA STESHENI YA SGR DAR

Na Mwandishi wetu TRC



Meneja Mradi wa SGR Dar es Salaam - Morogoro Mhandisi Machibya Masanja akitoa maelezo kuhusu maendeleo ya ujenzi wa Stesheni ya SGR katika eneo la Stesheni jijini Dar es Salam hivi karibuni Julai, 2020.

Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Bwana Paul Makonda afanya ziara katika Stesheni ya Reli ya Kisasa - SGR inayojengwa katika eneo la Stesheni jijini Dar es Salaam hivi karibuni Julai, 2020.

Lengo la ziara hiyo ni kukagua utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015 ambayo ilibainisha ukarabati wa reli ya zamani na ujenzi wa reli mpya ya kisasa ambayo utekelezaji wake umefika zaidi ya 84% kwa kipande cha Dar es Salaam - Morogoro na 32% kwa kipande cha Morogoro - Makutupora Singida.

Katika ziara hiyo Paul Makonda ameongozana na wasanii kutoka kampuni ya Wasafi Classic Baby wakiongozwa na Mkurugenzi wa Kampuni hiyo Nasib Abdul maarufu kama Diamond kwa lengo la kuhamasisha wasanii kuunga mkono jitihada za serikali ya awamu ya tano chini ya Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli za kuboresha miundombinu ya usafiri nchini.



Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Bwana Paul Makonda (mwenye suti) akiwa katika picha na baadhi ya viongozi wa Shirika la Reli Tanzania na wawakilishi wa Kampuni ya Yapi Merkezi katika Stesheni ya SGR jijini Dar es Salaam.

# WANANCHI WA KATA YA IHUMWA WAENDELEA KULIPWA FIDIA ILI KUPISHA UJENZI WA RELI YA KISASA



Na Mwandishi wetu TRC



Meneja mradi msaidizi kipande cha Morogoro - Makutupora Mhandisi Christopher Mang'wela akifafanua jambo kwa wananchi wa kata ya Ihumwa mkoani Dodoma waliofika katika zoezi la ulipaji fidia kupisha ujenzi wa reli ya kisasa hivi karibuni Julai 2020



Afisa Uhasibu kutoka Shirika la Reli Tanzania Bwana Nassor Ramadhan Said akimsainisha mmoja wa wakazi wa kata ya Ihumwa Bi. Catherine Suila kwa ajili ya kumpatia hundi wakati wa zoezi la ulipaji fidia kupisha ujenzi wa reli ya kisasa mkoani Dodoma hivi karibuni Julai 2020.

Shirika la Reli Tanzania laendelea na zoezi la ulipaji wa fidia kupisha ujenzi wa reli ya kisasa - SGR kipande cha Morogoro - Makutupora katika kata ya Ihumwa mkoani Dodoma hivi karibuni Julai 2020.

Katika awamu hii kiasi cha zaidi ya shilingi Bilioni moja kimetengwa ambapo watu 810 watalipwa wakati wa zoezi hilo litakalodumu kwa majuma mawili.

Hadi sasa jumla ya wakazi 231 wa kata ya Ihumwa wameshalipwa fedha zao ikiwa ni siku tatu tu tangu kuanza kwa zoezi hilo la ulipaji wa fidia kwa awamu hii.

Baadhi ya wakazi wa kata ya Ihumwa waliolipwa stahiki zao wameelezea furaha yao na shukurani kwa serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Jemedali Dkt. John Pombe Magufuli na Shirika la Reli kwa kuhakikisha wanapata fidia hizo.

Mmoja wa wakazi hao Bw. Dickson Chiwanga, amesema "naipongeza sana serikali kwa hatua hii kwani kitu wanachofanya ni cha kutuletea maendeleo na tutakitumia wote kwa pamoja"

Kuhusu matumizi ya fedha hizo, wananchi hao wameeleza kuwa fedha hizo zitawasaidia katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo ikiwemo biashara, kilimo, ufugaji na kuanzisha makazi mapya.

"hii pesa itanisaidia mambo mengi, kibiashara lakini pia naweza nikajenga hivyo naweza kutoka hatua moja kwenda nyingine" alisema Bw. Henry Shedrack,

Aidha wananchi hao wamewataka wenzao ambao bado hawajalipwa kupuuzia uzushi unaosambazwa na kuwa fedha hizo hazitalipwa na kusisitiza kuwa ni uongo na kwamba wote watalipwa haki zao kama ilivyokuwa kwao.

Zoezi hilo la ulipaji wa fidia linaendelea wakati ambapo mradi wa SGR kipande cha Morogoro - Makutupora, umefikia 38%

# TRC YASAINI MKATABA WA MAKUBALIANO NA WADAU KATIKA KUBORESHA MAISHA YA JAMII ZINAZOISHI PEMBEZONI MWA RELI

Na Mwandishi wetu TRC

Shirika la reli Tanzania – TRC limekutana na kutiliana saini mkataba wa makubaliano na wadau ili kuleta maendeleo katika jamii zinazoishi pembezoni mwa reli na wale ambao ardhi yao imetwaliwa na TRC kwa ajili ya kupisha mradi wa ujenzi wa SGR. Hafla imefanyika katika ukumbi wa TRC makao makuu jijini Dar es Salaam hivi karibuni Julai 29, 2020.

Lengo la hafla hiyo ni kuwakutanisha wadau tofauti ambao wamekuwa karibu na shughuli za utekelezaji wa miradi ya Shirika hususani Mradi wa Ujenzi wa reli ya Kisasa – SGR na Mradi wa Uboreshaji wa Reli ya Kati – TIRP na kujadili namna ya kupunguza athari hasi zinazotokana na miradi ili kuleta maendeleo kwa jamii zilizopo katika maeneo ya miradi.

Hafla hiyo imehudhuriwa na wadau tofauti zikiwemo taasisi za serikali ikiwemo kutoka Chuo kikuu cha Dar es Salaam - UDSM, Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi - VETA, Shirika la Maendeleo ya Viwanda vidogo - SIDO, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF, Wizara ya Mambo ya Ndani kupitia Jeshi la Polisi, Asasi zisizo za Kiserikali (NGO's), Kampuni ya Korail, Yapi Merkezi na Shirika la Uhandisi na Ujenzi la China – CCECC.

Aidha, mkataba huo pia umesainiwa kwa ajili ya kuendelea kuboresha maisha kwa jamii ambazo zinapatikana pembezoni mwa njia ya reli ambao unalenga kutoa msaada zaidi kwa kaya zilizopitiwa na mradi.

Mipango ambayo imeandaliwa kwa ajili ya kuboresha jamii ni pamoja na mafunzo ya usimamizi wa fedha kwa kaya zilizopitiwa na mradi, namna ya kupata ardhi na usalama wa umiliki, uboreshaji wa ardhi kwa kuongeza tija ya ardhi na kilimo, uhamaji wa mifugo na upatikanaji wa maji kwa mifugo, Kilimo na matumizi ya kawaida, kuasisi mpango wa uangalizi na usimamizi wa ukatili wa kijinsia pia kufahamiana ili kuendelea kushirikiana katika kushughulikia mambo yatakayojitokeza kwenye miradi.

TRC inatambua mchango mkubwa unaotolewa na taasisi hizi za jamii, hivyo TRC ina kila sababu ya kuongeza nguvu na ushirikiano wa karibu na taasisi hizi ili kuleta matokeo chanya katika utekelezaji wa miradi kwa kuwa miradi hii imeletwa ili kuleta faida kwa wananchi na si kuleta madhara.

Katika kuhakikisha malengo haya yanatimia TRC kwa kushirikiana na taasisi za serikali kama TASAF, SIDO, UDSM, VETA na zisizo za serikali (NGOs) zitahakikisha mambo ya kijamii, mazingira na kiuchumi yanakuwa sawa kwa wananchi wote walilengwa kwa mipango hii endelevu.

Wadau wametoa shukurani na pongezi kwa TRC kwa kufungua mkutano huo ambao utakuwa na manufaa makubwa kwa TRC na jamii inazozunguka mradi kupitia ushirikishwaji na makubaliano yaliyotiliwa saini katika mikataba hiyo.

TRC inatarajia ushirikiano mzuri kutoka kwa wadau na washiriki katika kutekeleza mipango iliyopendekezwa na kukaribisha mawazo mapya na uzoefu mbalimbali kutoka kwa wadau ili kuendelea kupata uelea wa pamoja na wadau ili kufanikisha utekelezaji wenye tija, ubora na ufanisi zaidi.




Kaimu Mkurugenzi Mkuu TRC Bi. Amina Lumuli (aliyeketi kati), wafanyakazi wa TRC wakiwa katika picha ya pamoja na wadau mara baada ya kumaliza mkutano uliofanyika katika ukumbi wa mikutano makao makuu TRC jijini Dar es Salaam hivi karibuni Julai 2020

# MATUKIO KATIKA PICHA



Na Mpiga Picha wetu TRC



Mchimbaji wa madini Bilionea Saniniu Laizer aliyepata mawe makubwa zaidi ya Tanzanite, akipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa kitengo cha Habari na UhusianoBi. Jamila Mbarouk, alipotembelea banda la Shirika la Reli Tanzania katika viwanja vya maonesho ya kimataifa ya biashara Saba Saba jijini Dar es Salaam hivi karibuni Julai 2020.



Meneja Mkuu wa Mkoa, wa Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia - TAZARA Ndugu Fuad Abdallah (kushoto) akipata maelezo kuhusu mfumo wa Usafirishaji wa reli ya kisasa kutoka kwa Afisa Usafirishaji Bi. Lucy Kingodi alipotembelea banda la TRC katika viwanja vya Saba Saba hivi karibuni Julai 2020.



Wananchi waliotembelea viwanja vya maonesho ya Biashara Saba Saba wakiwa katika foleni ya kuingia ndani ya banda la TRC kwa ajili ya kupata huduma na taarifa kuhusu miradi inayosimamiwa na TRC.



Baadhi ya wananchi waliotembelea banda la TRC katika viwanja vya Saba Saba wakipata maelezo kutoka kwa Afisa Uhusiano wa TRC Ben Mwanantala kuhusu maendeleo ya mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa, hivi karibuni Julai 2020.



Wananchi wakimsikiliza Mwanasheria kutoka TRC, Augustine Kulwa wakati wa kampeni ya ushirikishwaji wa jamii katika maendeleo ya mradi wa TIRP Kilosa mkoani Morogoro, hivi karibuni Julai 2020.



Kaimu Meneja Huduma kwa Wateja TRC Bi. Catherine Moshi akiwaelimisha wateja namna ya kukata tiketi kwa njia ya mtandao alipokuwa ndani ya treni ya kisasa ya Deluxe wakati wa safari Dar es Salaam – Kigoma hivi karibuni Julai, 2020

# MATUKIO KATIKA PICHA; MAONESHO YA SABA SABA



Na Mpiga Picha wetu TRC



Mtaalamu wa Masula ya Mawasiliano kutoka TRC Ivinary Sansa akitoa maelezo kuhusu mifumo ya mawasiliano katika mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa kwa baadhi ya wananchi waliotembelea banda la TRC katika viwanja vya Saba Saba jijini Dar es Salaam hivi karibuni Julai 2020.




Mwananchi aliyetembelea banda la TRC akisaini katika kitabu cha wageni katika viwanja vya maonesho ya Kimataifa ya Biashara Saba Saba jijini Dar es Salaam hivi karibuni Julai 2020.





Mhandisi Ujenzi kutoka TRC Faraja Yusto akielezea kuhusu mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR kwa wananchi waliotembelea banda la TRC katika viwanja vya Saba Saba jijini Dar es Salaam hivi karibuni Julai 2020.



Afisa Uhusiano kutoka TRC Ben Mwanantala akitoa maelezo kuhusu maendeleo ya mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa kwa baadhi ya wananchi waliotembelea banda la TRC katika viwanja vya Saba Saba jijini Dar es Salaam hivi karibuni Julai 2020.




Afisa Uhusiano kutoka TRC Hassan Said akitoa maelezo kuhusu maendeleo ya mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa kwa baadhi ya wananchi waliotembelea banda la TRC katika viwanja vya Saba Saba jijini Dar es Salaam hivi karibuni Julai 2020.




Afisa Uhusiano kutoka TRC Augustino Bulegea akitoa maelezo kuhusu maendeleo ya mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa kwa baadhi ya wananchi waliotembelea banda la TRC katika viwanja vya Saba Saba jijini Dar es Salaam hivi karibuni Julai 2020.




SHIRIKA LA RELI TANZANIA
Mtaa wa Reli/Barabara ya Sokoine
S.L.P 76959
Dar es Salaam
TANZANIA
Barua pepe; info@trc.co.tz
Tovuti; trc.co.tz
Simu ya Bure; 0800 110 042



Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano
SHIRIKA LA RELI TANZANIA

| | |
|---|---|
| MHARIRI MKUU | Jamila Mbarouk |
| MHARIRI MSAIDIZI | Sami Omary |
| MTAYARISHAJI | Sami Omary |
| MAKALA | Aziza Charles |
| HABARI | Tracylinda Nganga |
| PICHA | Seleman Kadiko |
| KIBONZO | Hassan Said |


tzrailways TRC Reli TV

Reli Yetu | Maendeleo Yetu | Taifa Letu #TRCMpya